
HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 10 January - April 2012

# Je kuna Tija ya Mapambano dhidi ya Umasikini kwa Biashara ya Hewa Ya Ukaa?

Dunia imekuwa katika mapambano dhidi ya uchafuzi wa mazingira ambao ni matokeo ya maisha ya binadamu kama vile ongezeko kubwa la watu na kukua kwa teknolojia katika viwanda. Kumekuwa na matamko, sera, sheria na mikataba mbalimbali katika ngazi ya kitaifa na kimataifa kuhusu kupunguza uchafuzi wa mazingira na hali ya hewa duniani. Aidha, kumekuwepo na jitihada katika ngazi ya Umoja wa Mataifa kama vile mkataba wa mwaka 1992 wa kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi na mkataba wa Kyoto wa mwaka 1998 uliozipa nchi zilizoendelea jukumu la kupunguza uchafuzi wa hewa na kuruhusu biashara ya hewa ukaa ili kupunguza mabadiliko ya tabia ya nchi.



*Uwiano kati ya mahitaji ya wenyeji na hifadhi ya mazingira uzingatiwe katika biashara ya hewa ya ukaa*

Mikataba ya kimataifa inasisitiza kanuni mojawapo ya mchafuzi wa mazingira kugharamia uhifadhi wa mazingira kanuni ambayo inaziwajibisha nchi zilizoendelea kiviwanda kufidia jitihada za nchi zinazoendelea katika kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti ambayo hufyonza hewa ukaa. Kwa hapa Tanzania, Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa kutokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMI) ndiyo mkakati wa kitaifa Endelea Uk.3

## NUKUU

*"Ni muhimu kila nchi kuzingatia uhuru, uelewa sahihi wa wanajamii kabla hawajaridhia mradi wowote wa MKUHUMI. Kama tararibu zote zitafuatwa na kama wanajamii wanakuwa wadau katika miradi ya MKUHUMI watafaidika kwa; ajira za utengenezaji vitalu vya miti, upandaji miti utunzaji na ulinzi wa misitu"*

## YALIYOMO

- Je kuna Tija ya Mapambano... Uk.1,3,5
- Tahariri Uk.2
- Biashara ya Hewa ukaa Uk. 4 - 5
- MKUHUMI na Mustakhabali 6 -7
- Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi Uk. 8
- Kona ya Sheria Uk. 9
- Safu ya maoni ya wasomaji Uk. 10
- Kukosekana kwa uwiano wa Maslahi Uk. 11

**ARDHI NI UHAI ni jarida la Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi (HAKIARDHI), ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mhariri**
Yefred E. Myenzi
Alice Shamge
Gloria Jimwaga

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe
Alice Shamge - Mjumbe

**Mchapishaji**
HAKIARDHI

**UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI**

WASOMAJI wa jarida hili mnakaribishwa kutoa michango yenu kwa kuuliza maswali, ushauri, maoni au kwa kuandika makala. (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani zifuatazo:

Mhariri:
**ARDHI NI UHAI**
**S.L.P 75885**
**Dar es Salaam**

Email:
**info@hakiardhi.org**

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

Email:
**ecoprinttz@yahoo.com**

# TAHARIRI

## Umakini bado katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi!


*Na Yefred Myenzi*

Katika toleo hili, tumechambua kwa undani kuhusu maana hasa ya biashara ya hewa ya ukaa namna inavyofanyika vigezo vinavyohitajika kwa nchi na wakulima wa miti kukidhi viwango pamoja na kuvinjari uhusiano kati ya biashara hii na vita dhidi ya umaskini na njaa. Inavyoelekea, nchi zilizoendelea zimejipanga sana kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabia nchi lakini kwa upande wetu hali inaonyesha kuwa hadi sasa ni kama tumedandia tu gari inayopita lakini hata hatujui linakoelekea kama taifa. Kokote watakakotupeleka wanaoendesha gari inaonekana ni sawa tu hata kama ni kwenye vilindi vya maji vyenye kina kirefu. Hatuko makini kabisa kama taifa na mambo ya msingi kwa uhai wetu kama hili la mabadiliko ya tabia nchi na mikakati ya kukabiliana nalo. Masuala matatu yanaweza kutusaidia kuendelea kutafakari kuhusu umakini wetu au kutokuwa makini kwetu.

Kwanza mabadiliko ya tabia nchi si porojo wala ndoto au masuala ya kijinamizi. Ni hali halisi inayotokea kama inavyodhihirishwa na mafuriko, ukame, majira yanayobadilika kila uchao, ongezeko la maradhi sugu n.k. Ili watanzania wapone na janga hili, hatuwezi kufika popote kwa kufanya miradi ya ruzuku za hewa ya ukaa kama inayoendelea sasa mikoa ya yanda za juu kusini. Ni lazima kuwekeza katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia na mitizamo yetu juu ya mazingira na uhifadhi wa uoto wa asili na kusimamia maamuzi yetu. Mwaka 2006, aliyekuwa Makamu wa Rais wa wakati huo alitoa waraka maalumu wa kulinda hifadhi ya vyanzo vya maji, ardhi oevu, misitu na maeneo yenye umuhimu wa kipekee wa kibaoanuai. Tangu wakati huo, serikali imekuwa ikivizia kuwatoa wafugaji mara bonde la Ihefu, mara Kilombero na kwingineko na baada ya muda mfupi operesheini inafungwa hadi miaka mingine sita ipite. Hatufiki kwa mtindo huu, ni lazima tumaamishe tunachokisema na kukisimamia kwa dhati kama kweli tunataka mabadiliko. Mtizamo huu wa kukabiliana na janga hili ni potofu na dhaifu.

Jambo la pili ni elimu. Hili limejadiliwa sana na mada za toleo hili lakini kikubwa ni kwamba ili watu wakabiliane na athari za mabadiliko ya tabia nchi, ni lazima wawe na uelewa wa kutosha wa janga lenyewe na ubora wa mbinu mbadala za kuondokana na tabia na vitendo vinavyochochea mabadiko ya tabia nchi. Kuacha kukata kuni wakati ndio chanzo pekee cha nishati si rahisi kwa mwananchi ila ikiivishwa kwa mbinu za kupata nishati mbadala ni rahisi tu.

La tatu, mfumo wa sera na sheria hauwekwi kwa ajili kulinda maslahi ya makampuni tu bali pia haki na stahili za wananchi. Ilivyo sasa, ni kama vile serikali imeyaachia makampuni binafsi kuendesha biashara ya hewa ya ukaa kwa kushirikiana na nchi wafadhili yanakotoka makampuni husika huku wananchi wakijikaanga wenywe kwa mafuta yao. Angalia jinsi ardhi ya kilimo inavyogeuza kuwa misitu na maafisa ardhi na kamishina wao wakitia bidii kuhawilisha ili makampuni yamiliki badala ya wananchi wao. Tusipokuwa makini kuwezesha wananchi kumiliki ardhi kwanza na kujihakikishia uwepo wa chakula, si muda mrefu pesa ya ruzuku ya hewa ya ukaa itakatika kama ilivyo kwa mipango mingine ya mpito, tutadondokea katika janga la kudumu la njaa. Tunayo nafasi kama taifa ya kujipanga kwa sheria, kwa elimu, kwa ushiriki wa watu wetu katika umiliki wa ardhi na uzalishaji na tukitaka, kuwawezesha kuwa wapandaji wa miti na wanufaikaji wa biashara ya hewa ya ukaa badala ya kusubiri kuwa manamba kwenye ardhi yao wenyewe wapate ujira usiokidhi hata kujikimu kwa chakula. Tuzidi kutafakari kama kweli mikakati yetu ya sasa iko sawa!

# Mapambano dhidi ya Umasikini

Inatoka uk. 1

unaowezesha nchi zilizoendelea kuchangia uhifadhi wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuchangia jitihada za utunzaji wa misitu ya asili na upandaji wa miti.

Chimbuko la MKUHUMI ni katika mkutano wa 11 wa nchi zilizoridhia mkataba wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi uliofanyika Montreal, Canada mwaka 2005 ambako umoja wa nchi zenye misitu ya mvua zikiongozwa na Costa Rica na Papua New Guinea ulipeleka maombi rasmi Umoja wa Mataifa wa kutaka nchi zinazoendelea kulipwa fidia kwa kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu. Hii ni kutokana na tafiti mbalimbali kuonyesha kuwa takriban asilimia 20 ya uchafuzi wa hewa husababishwa na uharibifu wa misitu na ukataji wa miti.

Mwaka 2007 katika mkutano wa 13 wa nchi zilizoridhia mkataba wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi uliofanyika Bali, Indonesia Kulipitishwa mkakati wa MKUHUMI chini ya mkataba wa Kyoto kwa malengo ya; kupunguza uchafuzi wa hewa kutokana na ukataji miti na uharibifu wa misitu, kuongeza hifadhi ya hewa ya Carbon katika misitu, kuendeleza mikakati endelevu ya uhifadhi wa misitu, na kutunza misitu. Hata hivyo MKUHUMI umefanyiwa marekebisho mawili nayo ni MKUHUMI+ na MKUHUMI++ ambayo yaliruhusu upandaji miti, na uzalishaji misitu. Mpango wa MKUHUMI unaruhusu nchi, miradi, jamii na mtu binafsi kupata ruzuku kutoka katika nchi zilizoendelea katika jitihada za kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu.

Mikataba ya Kimataifa inazitaka nchi zilizoridhia mikataba hiyo kuweka sera, sheria na taasisi zitakazosimamia taratibu za kuratibu MKUHUMI. Ni muhimu kila nchi kuzingatia uhuru, uelewa sahihi wa wanajamii kabla hawajaridhia mradi wowote wa MKUHUMI. Kama taratibu zote zitafuatwa na kama wanajamii wanakuwa wadau katika miradi ya MKUHUMI watafaidika kwa; ajira za utengenezaji vitalu vya miti, upandaji miti utunzaji na ulinzi wa misitu. Pia, jamii ikitunza miti vizuri na kuacha kuchoma misitu na kupanda miti mingi, inaelezwa kuwa mvua zitaongezeka, vyanzo vya maji vitadumu na misimu ya mvua haitabadilika ovyo.



Na Godfrey Massay

Aidha, inaelezwa kuwa, kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi kutakuza kilimo kwa jamii na mtu mmoja mmoja na hatimaye kuwezesha upatikanaji wa uhakika na usalama wa chakula miongoni mwa wanajamii. Na hatimaye kutakuwa na ustawi wa maisha ya wanajamii kutokana na fursa na manufaa mbalimbali kama vile malipo yatokanayo na biashara ya hewa-ukaa katika kuboresha huduma za kijamii kama vile shule, zahanati na barabara.

Bila shaka tathmini ya haraka ya manufaa na fursa hizo yanaweza kumuaminisha kila mtu kuwa mkakati huu kabambe ndio dawa ya umaskini kwa wananchi hasa wanaoishi maeneo yenye misitu na yanayofaa kupandwa miti ikastawi vizuri. Hata hivyo, yapo mambo mengi ya kujiuliza kabla ya kuamini moja kwa moja hasa kwa kuangalia hali halisi ya mazingira ya nchi kama Tanzania. Kwanza, kanuni na vigezo vinavyosimamia utaratibu mzima wa tathmini ya hewa ya ukaa inayofyonzwa na miti haviwapi fursa wazalishaji wa kawaida kunufaika na mchakato huu kwavile si sehemu ya majadiliano na tathmini ya utimizaji vigezo vinavyotolewa katika ngazi ya kimataifa. Pili, ardhi inayotakiwa kupanda miti si kiasi kidogo bali ni kubwa kwa maelfu ya hekta. Ardhi hii ama inamilikiwa na wananchi au haijapimwa kubainisha wamiliki wake stahili kwa sasa. Kwa kuangalia mienendo ya makampuni yaliyo katika sekta yenyewe, hii imekuwa fursa kwao kujipatia ardhi kutoka kwa wananchi ama bure au kwa malipo kidogo na

Endelea Uk.5



*Biashara ya hewa ya ukaa iboreshe huduma ya vyanzo vya maji kwa wananchi*



Na Valentin N. Olyang'iri

# Biashara ya Hewa ukaa isiathiri haki ya milki ya Ardhi kwa wenyeji



Na Bhoke Matiku

Katika miaka ya karibuni, dunia imeshuhudia majanga yanayosababishwa na ongezeko la jotoridi na mafuriko kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Majanga haya yamechochea jitihada za mataifa mbalimbali kujadili hatma ya dunia na watu wake katika kujinasua na hatari zaidi. Tafiti zinaonyesha kuwa wachafuaji wakubwa wa mazingira na hali ya hewa ni mataifa yaliyoendelea ya Ulaya na Amerika Kaskazini lakini waathirika wakubwa wa mabadiliko ya tabia ya nchi ni nchi zinazoendelea katika mabara ya Afrika, Asia na Amerika Kusini.

Ni kweli kuwa suala la mabadiliko ya tabia ya nchi ni suala la dunia nzima kutokana na athari zake kuathiri kila eneo la nchi. Kwa maana hiyo hata mikakati ya kukabiliana nayo imekuwa ni ya pamoja baina ya mataifa yaliyoendelea na yanayoendelea. Kwa mfano mkutano kimataifa wa mazingira wa Rio de Janeiro wa mwaka 1992 ulioamua kuwa ni lazima nguvu za pamoja zitumike katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi. Vile vile mkutano wa Kyoto, Japani wa mwaka 1998 uliotoa mwongozo wa juu ya nini kifanyike kukabiliana na mabadiliko ya hewa ukaa ikiwemo kuanzishwa kwa MKUHUMI ili kupunguza hewa ya kaboni angani inayosababishwa na ukataji, uchomaji wa misitu na ongezeko la gesi chafu toka viwandani.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo linatahadharisha kuwa misitu imeendelea kuharibiwa zaidi duniani hasa katika ukanda wa Afrika, Amerika ya Kusini na Bara Hindi ambapo ripoti kutoka Umoja wa Kimataifa zinaonyesha uharibifu wa misitu kwa wastani wa hekta milioni 13 kuanzia mwaka 1990-2005. Katika kukabiliana na ongezeko la mabadiliko ya tabia ya nchi, Umoja wa Mataifa umeendelea kutafuta uungwaji mkono kwa nchi mbalimbali katika kutia saini makubaliano ya Kyoto ingawa nchi zilizoendelea kwa viwanda zimebakia nyuma kutia saini makubaliano hayo. Hadi sasa ni nchi 29 kutoka Afrika, Amerika ya Kusini na Asia, ambapo nchi 12 kati ya hizo, ikiwemo Tanzania, zinapata msaada ili kutekeleza mpango wa MKUHUMI, na kufikia mwaka 2011, zaidi ya dola za Kimarekani milioni 500 zimetengwa kwa miradi ya majaribio katika nchi tisa ikiwemo Tanzania.

Biashara ya hewa ya Ukaa inatokana makubaliano ya Kyoto ambapo nchi zinazotoa gesi ya kaboni na gesi nyingine kwa wingi zaidi zimekubali zenyewe kupunguza kiwango cha gesi hadi kufikia mwaka 2012. Kulingana na Mpango Mkakati wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabia nchi, kadri kiwango cha utoaji wa gesi chafu kinavyopopungua ndipo kampuni inapopata kiwango cha fedha kwaajili ya hewa ukaa na pesa hutolewa tu kwa kampuni ambazo nchi zao zimetia saini mkataba wa Kyoto.



Milki ya ardhi uwezeshe matumizi mseto kama haya

Biashara ya hewa ya Ukaa imeingia katika nchi za Kiafrika ikiwemo Tanzania kwa takribani miongo miwili sasa, ambapo kampuni kutoka nchi zilizoendelea ambazo zimetia saini au kuridhia Mkataba wa Kyoto zinapaswa ziwe na matawi yake katika nchi zinazoendelea ili ziweze kupanda misitu na kuweza kukidhi viwango vya utoaji wa pesa za kaboni. Nchini Tanzania, tumeshuhudia kampuni kutoka nchi zilizoendelea mfano Green Resources Limited kutoka nchini Norway na kampuni ya New Forest ya Uingereza zikichukua ardhi kubwa vijijini kwa lengo la kuhifadhi misitu na kupanda miti ili ziweze kunufaika na biashara ya hewa ya ukaa.

Pamoja na jitihada zote hizo ambazo zina mantiki kwa mazingira na kimataifa, swali la kujiuliza ni kwa kiasi gani haki za ardhi za wananchi wa vijijini wanaotoa ardhi zao kwa ajili ya upandaji wa miti zitalindwa. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa wimbi la utoaji ardhi kwa uwekezaji mkubwa sio tu katika biashara ya hewa ya ukaa lakini katika Nyanja nyingine limefungua ukurasa mpya wa uporaji wa haki za wenyeji juu ya ardhi ambayo wamekuwa wakitumia maisha yao yote kujikimu.

Pili, katika kugawa ardhi, tofauti na madai kuwa ardhi isiyo na rutuba na isiyofaa kwa kilimo ndiyo inayochukuliwa, tafiti zinaonyesha kuwa ardhi yenye rutuba ndiyo hasa inayolengwa. Katika baadhi ya maeneo ya wilaya ya Kilolo ambako upandaji miti umepamba moto, hata maeneo ambayo wenyeji huyatumia kwa kilimo cha msimu wa mvua hafifu kabla ya msimu wa kilimo kuanza maarufu kama vinyungu nayo yamechukuliwa na kupandwa miti. Ieleweke kwamba maeneo haya licha ya rutuba, pia huhifadhi maji kwa muda mrefu kwavile yako mabondeni.

Tatu, maeneo yanayotolewa ni makubwa na kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizokwisha fanywa na Endelea Uk.5

# Mapambano dhidi ya Umasikini

*Inatoka uk. 3*

kujipatia faida kubwa bila kujali matumizi ya awali ya ardhi hiyo kwa wananchi ikiwemo uzalishaji wa chakula. Tayari baadhi ya vijiji vimeingia mikataba ya kutoa ardhi kubwa kufikia hadi hekta 11,000 bure huku manufaa yanayoelezwa katika mikataba na makampuni husika ikihusisha asilimia 10 tu ya pato la faida kwenda kwa wananchi kiasi ambacho hakilingani na thamani halisi ya ardhi katika kipindi cha zaidi ya miaka 15 ya mikataba husika.

Katika mazingira kama haya ambayo ardhi inaweza kutolewa bila kujali kwanza mahitaji halisi ya wananchi hasa kwa matumizi yao ya asili ya kuzalisha ili kujipatia kipato cha kujikimu, ni dhahiri kwamba jitihada binafsi za kupambana na umaskini wa kipato zinafifia taratibu kwa kukimbilia mikakati mipya ambayo haijapangiliwa vizuri. Aidha, ajira za muda mfupi za utengenezaji vitalu vya miche, kupanda miti na kulinda misitu ambazo zinafurahiwa, zinafifisha jitihada za wananchi kufanya kazi zao binafsi za kujipatika kipato cha maana zaidi ya kuwa vibarua wa malipo kidogo kama ilivyo sasa.

Ni dhahiri kwamba serikali ina wajibu mkubwa katika hili. Kwanza ni katika kuweka sera na sheria madhubuti ambazo zitalinda rasilimali za nchi na wananchi wenyewe ikiwa ni pamoja na kuweka mgawanyo sawa baina ya makundi mbalimbali ya wenye maslahi katika rasilimali hizo ili kuwezesha wananchi waishio maeneo yenye rasilimali hizo kutopoteza fursa ya kuendelea na uzalishaji eti kwa kutegemea mgao wa pesa kutokana biashara ya hewa ya ukaa inayofanywa na makampuni. Pili, kuwaandaa wananchi kwa uelewa na ujuzi unaotakiwa ili wawe washiriki wanufaikaji wa miradi hii ili kuepukana na kudanganywa kunakotokana na uelewa hafifu wa mipango na biashara kama hii.

Katika ngazi ya kimataifa bado kuna changamoto nyingi kama vile; nchi zilizoendelea kutokutimiza wajibu wake wa kupunguza uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa hewa kutokana na uzalishaji katika viwanda vyao. Ni vema serikali ikaelekeza jitihada katika kudai uwajibikaji mkubwa zaidi wa nchi hizi na makampuni yao yenye maslahi ya kiuwekezaji katika sekta hii ili kuhakikisha kuwa nchi zinazoendelea zinapata malipo kutokana na juhudi zao za kutunza mazingira ambazo kwa baadhi ya maeneo kama Njombe, Mufindi na Kilolo ni sehemu ya utamaduni wao Vinginevyo, biashara ya hewa ya ukaa itabaki kuwa kiini macho kwa jitihada za kupambana na umaskini endapo wenyeji wanashiriki kwa kugawiwa pesa badala ya kuwezeshwa bila kunyang'anywa ardhi iliyo nyenzo yao ya kujikimu na kupambana dhidi ya umaskini.

# Biashara ya Hewa ukaa isiathiri haki ya milki ya Ardhi kwa wenyeji

*Inatoka uk. 3*

zinazoendelea, utoaji wake kwa wawekezaji unahusishwa na ahadi tamu za kufaidika na uwekezaji wa miti katika maeneo hayo. Hata hivyo, ukiacha ujira wanaopata vibarua na fidia iliyolipwa mara moja kwa baadhi ya wenye maeneo, faida za muda mrefu za moja kwa moja kwa wananchi hasa kutokana na kutoa ardhi yao hazipo maana ni sehemu chache sana kama vile kijiji cha Idete Wilaya ya Mufindi ambako mwekezaji aliingia mkataba na kijiji ambao hata hivyo hausemi lolote kuhusu umiliki wa ardhi.

Nne, suala la uhamishaji wa milki kutoka kwa wananchi kwenda kwa mwekezaji kulingana na taratibu zilizo katika sheria ya ardhi ya vijiji ya 1999 limekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi hasa kutokana na ukweli kuwa wengi wao hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na uhawilishaji wa ardhi ya kijiji kuwa ya jumla hususani ushiriki wao katika vikao halali vya mkutano mkuu ambavyo vina dhamana ya kufanya maamuzi ya mwisho ya kukubali au kukataa uhawilishaji kulungana na maslahi kwa kijiji na wanakijiji. Fursa hii inaonekana kutumiwa vilivyo na watendaji katika ngazi za vijiji, Kata na Halmashauri ya Wilaya kupitisha maamuzi bila kujali tija kwa wananchi vijijini wala mustakabali wao kwenye ardhi ambayo ndiyo rasilimali pekee wanayoitegemea kuendeleza maisha yao.

Hivyo basi, pamoja na kutambua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kwenye maisha ya binadamu ni muhimu pia kutambua kuwa mikakati ya kukabiliana na athari hizi isipotekelezwa kwa umakini hasa katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, basi matatizo yatakuwa ni makubwa zaidi. Kuna kila dalili kuwa mikakati hii itasababisha uhaba mkubwa wa ardhi miongoni mwa wananchi nchini hasa ardhi inayofaa na kutumiwa kwa uzalishaji. Lakini vilevile athari za madawa yanayotumika na makampuni ya kimataifa katika kukuzia miti ili kupata faida ya haraka zitakuwa kubwa sana katika afya za wananchi hawa wasiokuwa na elimu ya kutosha ya kujikinga wala kuchukua tahadhari.

Ni muhimu basi kwa Serikali na wadau wengine kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa mafunzo ya kutosha ya kulinda, kutumia na kuhifadhi rasilimali za ardhi badala ya kutoa maeneo makubwa kwa wawekezaji na wao kuishia kuwa vibarua, na kukosa ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na hata makazi. Hilo litawezekana tu pale ardhi ya vijiji ikifanyiwa mpango wa matumizi bora na kuwekewa sheria ndogo ndogo kama inavyoelekezwa katika sheria za ardhi kwa matumizi endelevu na manufaa ya vizazi vijavyo.

Ardhi ni Uhai January - April 2012

# MKUHUMI na Mustakhabali wa Milki ya Kimila



Na Knut Christian Myhre


MKUHUMI ni jitihada za kimataifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaathiri ustawi wa maisha ya watu duniani pote. Ni vyema itambulike kuwa idadi kubwa ya watu wanaoathirika na uchafuzi wa mazingira sio wao wanaochafua mazingira yenyewe. Kwa mfano wananchi barani Afrika ni waathirika wakubwa wa uchafuzi huu lakini wachafuzi wakubwa ni wamiliki wa viwanda vikubwa huko Ulaya na Amerika.

Ni sahihi kusema kuwa mabadiliko ya tabia ya nchi yana madhara makubwa kwenye maendeleo ya wananchi lakini mikakati ya kupambana nayo kama vile MKUHUMI itakapotekelezwa isivyo sahihi basi itakuwa na madhara makubwa zaidi kwa wananchi wa nchi maskini kama Tanzania. Kwa mfano upandaji wa miti kwajili ya kufyonza hewa ukaa ni chanzo kimojawapo cha kusababisha uhaba na uhakika wa chakula pamoja na kupunguza uhakika wa wananchi kumiliki ardhi zao endapo mkakati huu hautatekelezwa vizuri.

> **Katika maeneo mengi ya vijijini kwa sasa kuna migogoro ya ardhi inayotokana na uhaba na ugawaji holela wa ardhi kwa wawekezaji wakubwa bila kuzingatia matakwa na mahitaji ya wenyeji.**

Kwa nchi kama Tanzania ambayo ina aina ya umiliki wa ardhi wa kimila ni muhimu sana kuchukua tahadhari katika utekelezaji wa mkakati huu. Kwa mujibu wa sheria za ardhi, ardhi ya kijiji inamilikiwa kimila lakini pindi inapotolewa kwa uwekezaji inakuwa inamilikiwa kama ardhi ya jumla ambayo umiliki wake sio wa kimila. Kwa maana hiyo umiliki wa kimila unakuwa umepoteza thamani na wanavijiji wanakuwa hawana mamlaka nayo tena.

Nimesoma vizuri sana taarifa ya Tume ya Rais ya miaka ya 90 maarufu kama tume ya Shivji. Lengo la mapendekezo ya Tume hii la ardhi ya vijiji kumilikiwa kimila chini ya vyombo vya wananchi wenyewe ambavyo ni Mkutano Mkuu wa Kijiji na Halmashauri ya kijiji lilikuwa ni kupambana na utandawazi ambao ungekuwa chanzo cha uporaji wa ardhi ya vijiji. Tume ilitambua kuwa Maendeleo ya kiteknolojia na kiviwanda yangesababisha ardhi ya Afrika kuwa sehemu ya pekee ya nchi za Ulaya na Amerika kutatua matatizo yake ya kiuchumi na kisiasa.



Uchomaji moto na ukataji miti hovyo kama huu unachangia kuharibu uoto wa asili

Pamoja na mapendekezo mazuri ya Tume na sera na sheria za ardhi kutungwa mwaka 1995 na 1999, bado kumekuwa na ukiukwaji wa haki za ardhi za wazalishaji wadogowadogo kwenye vijiji. Mfumo wa sasa unaonyesha kutoweka uwiano wa kiutendaji ambao unaharibu utaratibu wa kimila na kutukuza umiliki wa kisheria hali inayowanyima wanavijiji haki zao. Kwa mfano ardhi yote ya kijiji iko chini ya mamlaka ya Mkutano Mkuu wa Kijiji lakini maamuzi kuhusu ugawaji wa ardhi inayozidi ekari 50 yapo chini ya Halmashauri ya Wilaya, wakati maamuzi ya ugawaji zaidi ya ekari 250 yapo chini ya Kamishina wa ardhi. Vilevile Rais anayo mamlaka ya milki ya hatma juu ya ardhi na uwezo wa kuhawilisha matumizi ardhi kutoka ardhi ya kijiji kuwa ama ya hifadhi au ya kawaida na pia kutwaa ardhi yoyote iwe ya kijiji, jumla au hifadhi kwa manufaa ya umma. Matokeo yake nguvu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji na umiliki wa kimila vinaishia katika sehemu ndogo ya ardhi yaani ekari 50 wakati mamlaka juu ya ardhi yote yapo katika ngazi ya wilaya na taifa, ambazo zinamilikiwa kwa utaratibu wa sheria.



Ulishaji mifugo uzingatie hifadhi ya mazingira

Matokeo ya mfumo huu wa kisheria umeruhusu utandawazi ambao Tume iliweka mikakati ya kukabiliana nao. Mfano mkakati wa kupunguza hewa ya ukaa unaweza kuwa mbinu mojawapo ya kupunguza wigo wa wanavijiji kumiliki ardhi kimila. Hii inatokana na ukweli kuwa hakuna mwekezaji atakayependa kupanda msitu mkubwa katika ardhi asiyokuwa na hati nayo hivyo lazima atataka ihawilishwe tendo ambalo lazima limpore mmiliki wa asili.. Katika maeneo mengi ya vijijini kwa sasa kuna migogoro ya ardhi inayotokana na uhaba na ugawaji holela wa ardhi kwa wawekezaji wakubwa bila kuzingatia matakwa na mahitaji ya wenyeji .

Ni vizuri kuchukua tahadhari katika utekelezaji wa MKUHUMI katika kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa sehemu ya umiliki wa ardhi itakayotumika kwa ajili ya upandaji wa miti na misitu. Ni lazima mfumo wa sheria za ardhi nchini uweke mbele haki za ardhi za wazalishaji wadogo dhidi ya maslahi ya wawekezaji wakubwa. Kuwekwe ukomo wa ardhi ya vijiji inayotumika katika kupanda miti ili kuepusha athari za upungufu wa chakula wakati ujao.

Mchakato wa utungwaji wa katiba mpya ya nchi unatoa fursa ya kuitazama upya mifumo isiyofuata usawa katika usimamizi na umiliki wa rasilimali. Ni wakati wa kuzipa mamlaka za vijiji maamuzi ya ardhi katika maeneo yao kama Tume ya Shivji ilivyopendekeza. Utawala wa ardhi ya vijiji na utatuzi wa migogoro unatakiwa ujikite katika utaratibu wa kimila bila kuingiliwa na mifumo ya kirasimu. Kwa njia hii utaratibu wa kimila unaweza kuwa chanzo cha uhakika wa umiliki wa ardhi kwa wazalishaji wadogo wadogo nchini.

# Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi kwa wazalishaji wadogowadogo nchini; Elimu zaidi inatiakiwa



Na Joseph Chiombola



Na Beatha Fabian

Mabadiliko ya mwelekeo wa hali ya hewa yamefanya sekta ya kilimo nchini kujitabanaisha kimkakati ili kuhakikisha kwamba sekta hiyo inaendelea kukua na kuchangia katika uchumi wa taifa. Kwa hali ilivyo sasa ukame wa muda mrefu na mafuriko yamefanya maisha ya wakulima wadogo, ambao hawana huduma za umwagiliaji, kuwa magumu zaidi.

Mvua fupi ambazo zinanyesha kati ya mwezi Aprili na Julai zimekuwa si za uhakika, joto limeongezeka kupita kiasi na ukame kwa maeneo mengi imeshakuwa hali ya kawaida. Hali hii imepelekea wazalishaji wadogo wadogo nchini kukosa uhakika wa lini wanapaswa kuandaa mashamba kwajili ya kupanda na lini wanaanza kupanda.

Hali ya hewa haitabiriki tena na hivyo kupelekea athari za mavuno ya kilimo ya wazalishaji wadogo.Tunatambua kwamba baadhi ya wakazi wa vijijini ambao ndio maskini wameathirika zaidi ukizingatia kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wanategemea sekta ya kilimo katika kuendesha maisha yao. Hali kadhalika, sekta ya kilimo inakadiriwa kuchangia takribani asilimia 60 ya mauzo ya nje.

Ripoti ya mwaka 2009 ya Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo inaonya kuwa Tanzania ina miongo miwili ya kukifanya kilimo kuendana na mabadiliko ya tabia nchi ama sivyo itakuwa katika hatari ya kushuka kwa pato la ndani la taifa.


Wataalam wa mabadiliko ya tabia nchi wanakubaliana kuwa njia pekee ya kuzuia madhara makubwa ya uchumi ni kubadili jinsi kilimo kinavyoendeshwa. Njia pekee ni kuelimisha wakulima kutumia mbinu bora za kilimo. Elimu inayotakiwa kutolewa ni ya kuhamasisha wakulima juu ya njia mbadala za kilimo kama vile kupanda mazao kwa mzunguko, kufuga mifugo ndani na kuzalisha mazao yanayohitaji maji machache na kustahimili ukame

Kwa upande mwingine inatabiriwa kuwa joto lina uwezekano wa kuongezeka kati ya nyuzi joto mbili hadi nne ifikapo mwaka 2100. Huu unaonekana kuwa muda mrefu, lakini inaonyesha kuwa mimea ya msimu kama vile mahindi na maharage hayataweza tena kukua na inabidi nafasi yake ichukuliwe na mazao ya mtama na uwele. Uzalishaji wa mahindi, zao kuu la chakula nchini Tanzania, unatarajiwa kushuka kwa theluthi moja katika miongo michache ijayo. Hii ni kutokana na zao hilo kuhitaji maji mengi mno. Katika maeneo ya kati ya nchi ambayo ni makavu zaidi, mavuno ya mahindi yanaweza kupungua kwa asilimia 84.

Wakulima pia wameshuhudia madhara ya mabadiliko ya mwelekeo wa mvua. Mahindi hayastawi tena vizuri, na kupelekea wazalishaji wadogo wadogo kubadili aina na mfumo wa mazao kwa kupanda mazao mengine kama vile mihogo na viazi vitamu ambayo hayahitaji mvua nyingi, ili waweze kuishi. Vilevile mabadiliko ya hali ya hewa yamezuia wakulima katika maeneo mbalimbali nchini kupanda maharage, kahawa, dengu na viazi vitamu kutokana na kuongezeka kwa wadudu waharibifu kutokana na kuongozeka kwa joto.

Kutokana na kuendelea kwa mabadiliko ya tabia nchi wazalishaji wadogo wataendelea kuathirika kwani kasi ya mvua kupungua au kutotosha, na kunyesha kwa wakati muafaka imekuwa ikiendelea na hiyo kuathiri uzalishaji wa mazao. Wakati mwingine, mvua hizi zimekuwa nyingi kupita kiwango hadi kusababisha uharibifu wa mazao.

Bila shaka sisi wote tunahusika kwa namna moja au nyingine katika kukabiliana na janga hili la kidunia. Wajibu wetu ni kubadili mifumo ya maisha yetu kuanzia namna ya kuandaa mashamba yetu, kuzalisha, kuvuna na kuhifadhi mazao. Kwa wafugaji kadhalika, wana wajibu mkubwa wa kuangalia namna idadi ya mifugo yao inavyoweza kupukutika kwa kasi ya hadi 800,000 kwa ukame wa mwaka mmoja tu na hivyo liwe funzo kwao kufuga kulingana na upatikanaji wa rasilimali ardhi, maji na huduma za mifugo. Ukiongeza na jitihada za matumizi ya njia mbadala za kilimo na aina ya mazao pamoja na harakati za kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kimataifa, dunia itaendelea kuwa mahali salama pa kuzalisha na kuendelea kuishi kwa vizazi na vizazi.



Ufugaji wenye tija sharti ujali hifadhi ya mazingira ili kuepuka ukame kama inavyoashiria kwenye picha hii

*Kona ya Sheria*

# Taratibu za kujisajili katika biashara ya soko la hewa ya ukaa



Na Joseph Chiombola

Biashara ya kimataifa ya hewa ya ukaa ni matokeo ya mikutano mbalimbali ya hali ya hewa iliyofanyika duniani ambapo mawazo ya MKUHUMI yalijitokeza katika mkutano wa Kyoto. Mkutano huo wa Kyoto uliridhia kwamba nchi za kaskazini na kusini ni lazima zipunguze athari za mabaliko ya tabia nchi mapema.

Ili kuweza kuingia katika biashara ya kimataifa ya hewa ya ukaa ni lazima nchi husika iwe imesaini kuridhia mkataba wa Kyoto. Vilevile mradi wa hewa ya ukaa ni lazima ufikie viwango vya maendeleo endelevu vya nchi husika na matokeo yake yaweze kuonyesha kiasi cha hewa ya ukaa kinachopungua angani. Mradi wa hewa ya ukaa unahusisha taratibu tano ili kuweza kujisajili na mwishowe kupata krediti kutokana na unyonyaji wa hewa ya ukaa angani. Taratibu hizo ni kama ifuatavyo;

### 1. Kuandika mradi
Katika hatua hii kuna uandishi wa mradi mzima utakavyokuwa kwa kuanisha kiwango cha hewa ya ukaa kinachotazamiwa kupunguzwa hewani na mradi pamoja na faida za kimazingira na kijamii. Vile vile mradi ni lazima uendane na viwango mbalimbali vya kimataifa vilivyowekwa.

### 2. Usanifu wa mradi
Katika hatua hii mradi huandikiwa maelezo ya kina na kuanishwa muda wake, namna za kufanya utafiti wa awali huanishwa na makadirio yake. Vile vile mfumo wa usimamizi huanishwa, tathmini ya athati za kimazingira na kijamii hufanyika pamoja na kukusanya maoni ya wadau.

### 3. Kupitishwa mradi
Baada ya usanifu kukamilika ni lazima mradi upitishwe na mamlaka ya kitaifa kama ilivyoainishwa katika mkataba wa Kyoto. Vilevile mwendelezaji wa mradi atahitajika kuupeleka mradi kwa mamlaka huru iliyosajiliwa na inayotambulika na Bodi ya wakurugenzi wa soko la hewa ya ukaa ili kuweza kuupitia mradi kujiridhisha na shughuli za mradi na kuangalia kiasi cha hewa ya ukaa kitakachopunguzwa na mradi na kisha huandika ripoti yake ya tathmini kwa Bodi ya Wakurugenzi.

### 4. Kusajiliwa mradi
Mara baada ya mradi kupitishwa na mamlaka huru maombi ya kuusajiri mradi yanaweza kupelekwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi wa soko la hewa ya ukaa au soko la hiari la hali ya hewa ambapo ripoti ya mamlaka huru ya tathmini na kibali cha mamlaka ya taifa huhitajika kupitiwa ili mradi uweze kusajiliwa.

### 5. Kupata Krediti na Malipo
Mara baada ya mradi kuanza, ili kuhakikisha ni endelevu ni lazima kuwe na uhakiki wa mradi kuaofanyika katika ngazi mbalimbali za utekekezaji wa mradi. Uhakiki huu hufanywa na mamlaka huru iliyosajiliwa na kutambulika na baada ya kujiridhisha kuwa mradi umekidhi viwango katika hatua zote za utekelezaji wa mradi krediti hutolewa na malipo hufanywa kwa mwendelezaji wa mradi.

Pamoja na taratibu hizo zilizoainishwa hapo juu yapo mambo muhimu yanayoangaliwa ili kuweza kupata motisha hiyo ya kifedha kutoka katika soko la hewa ya ukaa. Mambo hayo ni pamoja na Ongezeko, Uvujaji na Hali ya kudumu ambazo zimeanaishwa ifuatavyo:

- Ongezeko linazingatia ongezeko kwenye shughuli zinazoendelea tayari au zilizopangwa zinakidhi kufikiriwa kupata malipo ya kaboni. Kuendeleza shughuli zilizopo kama vile mipango mizuri ya kuhifadhi misitu na hifadhi siyo ongezeko kwahiyo mdai wa malipo ya kupunguza gesi joto ni lazima athibitishe shughuli hizi zisingefanyika kwa kutokuwepo mfumo wa soko la kaboni.
- Uvujaji maana yake ni kuongezeka uzalishaji hewa ukaa (kutokana na ukataji na uharibifu misitu) nje ya eneo la mradi wa MKUHUMI kutokana na kuwepo kwa shughuli za mradi.
- Hali ya kudumu ni dhana inayohusiana na muda wa matokeo ya shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Hii ina maanisha kuwa matokeo ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi hudumu milele ambapo katika hali ya kawaida huwa haiwi hivyo. Suala la udumu linaweza kubainishwa kwa kuangalia kiwango cha uzalishaji wa hewa ukaa iliyoko angani.

**Pamoja na nafasi ya maendeleo ya kiuchumi kutokana na motisha inayotolewa na soko la hewa ya ukaa zipo changamoto mbalimbali ambazo zinaambatana na biashara hiyo kama ifuatavyo;**

### 1. Gharama
Jamii nyingi zilizopo vijijini ambapo miradi hii inatekelezwa hazina uwezo wa kumudu gharama za hatua zilizoainishwa hapo awali. Ili kuweza kuundaa mradi inahitajika fedha ya kuwezesha kuandika mradi na pia kulipia gharama za wataalamu amabo watahusika katika kuuhakiki na kuhakikisha kuwa ni endelevu. Vilevile katika ukaguzi kabla ya malipo hayajafanyika kuna gharama za kuwalipa wanaokuja kufanya uhakiki kuwa miti yako imekidhi viwango vya kuweza kulipwa ambapo kwa sasa hakuna kampuni yeyote ya kitanzania yenye uwezo wa kufanya hii tathmini hivyo kulazimu kutumia huduma za makampuni ya nje ya nchi ambayo ni ghali sana.

### 2. Hitaji la hati
Mkaguzi anayekuja kukagua mradi wakati wa kuanzishwa na pia wakati wa maendeleo ya mradi na malipo ni lazima ahakikishe ya kuwa mradi umewekezwa katika ardhi yenye Hati. Changamoto kubwa hapa ni kuwa ardhi ya kijiji inamilikiwa kwa misingi ya kimila na utaratibu wa kumiliki ardhi kwa cheti cha hatimiliki ya kimila haukubaliki katika soko la hewa ya ukaa hivyo nafasi ya mwananchi wa kijijini kunufaika moja kwa moja na mradi ni finyu.

Kutokana na changamoto ya kifedha na hitaji la hati wananchi wengi wa vijijini hawawezi kumudu kuundesha mradi na ndio maana biashara hii kwa sasa inaendeshwa na makampuni makubwa kutoka nje na baadhi ya Asasi za kiraia nchini ambazo huendesha miradi na kisha kulipwa hela katika soko na kisha kotoa sehemu ya mapato katika jamii za vijiji zilizohusika na mradi hivyo jamii hazina uhusika wa moja kwa moja na soko ziadi ya kushirikishwa.

Hofu kubwa pia ambayo inaambatana na biaishara hii ni upungufu wa chakula kwa kuwa jamii nyingi kwa sasa zimeelekeza juhudi zake katika kutoa sehemu kubwa ya ardhi amabayo ilikuwa ikitumika au iliyotakiwa kutumika kwa kuzalishia chakula kwa ajili ya upandaji wa miti. Jamii hizi zimekuwa zikiishi kwa kutegemea hela ya motisha inayotolewa na soko la hewa ya ukaa ambayo hutolewa kwa hayo makampuni yanayoendesha mradi na kisha sehemu ya gawio ndio hutolewa kwenye jamii.

Licha ya kuwa soko la hewa ya ukaa linaweza kuwa fursa kwa jamii kupambana na umaskini lakini ni vema serikali ikaandaa mazingira bora ya sera na sheria zinazoratibu biashara hii ili mwananchi wa kawaida anufaike moja kwa moja badala ya kusubiri madalali. Ni vema pia taratibu za kawaida za uendeshaji wa biashara hii zikaangaliwa ili kuondoa ushiriki wa moja kwa moja wa makampuni makubwa ya nje hasa katika ardhi za vijiji maana ni dhahiri kwamba yananufaika zaidi kwa mgongo wa wananchi maskini wa vijiji husika huku nchi zao zikihusika pia kuendelea kuchafua mazingira na kuchangia athari za mabadiliko ya tabia nchi.

# Safu ya maoni ya wasomaji



## Mabadiliko ya Tabia ya Nchi

*PAMELA MASSAU (CARITAS, DAR ES SALAAM)*

Mabadiliko ya tabia nchi ni kitu ambacho haikiepukiki na ni lazima nchi zishirikiane katika kupunguza hewa ya ukaa, lakini kabla ya yote ni lazima maeneo yatengwe kwa kufuata utaratibu wa sheria na haki kwa wazalishaji wadogo ili yajulikane kama ni maeneo ya malisho, kilimo, hifadhi, n.k. Ni lazima wazalishaji wadogo wafaidike na kushirikishwa moja kwa moja na huu mpango wa MKUHUMI bila kusahau kutoa elimu shirikishi kwa jamii nzima.


## Athari za mabadiliko ya tabia nchi

*Haika Mcharo (Envirocare, DAR ES SALAAM)*



Athari za mabadiliko ya tabia nchi ni kubwa hasa kwa nchi zinazotegemea kilimo kama mfumo wa kiuchumi, lakini kiuhalisia asilimia kubwa za nchi zinazosababisha mabadiliko haya ni nchi zilizoendelea. Kwa mradi kama wa MKUHUMI unaohusu uuzaji wa hewa ya ukaa ni lazima ulenge kumfaidisha mwananchi mmoja mmoja. Changamoto ya huu mradi ni kwamba wananchi hawafaidiki moja kwa moja ukiangalia ngazi za utekelezaji ni ndefu kiasi cha kwamba hailengi kumfaidisha mzalishaji mdogo mdogo moja kwa moja, pia wananchi wengi hawana elimu ya kutosha juu ya hili swala, wanakijiji wanaambiwa wapande bila kuangalia mahitaji yao ya chakula kwanza hali inayoweza kusababisha upungufu wa chakula nchini. Napenda kushauri utekelezaji wa MKUHUMI uzingatie kumfaidisha mwananchi kulingana na thamani ya muda na miundombinu anayo wekeza kwenye misitu hiyo, pia ni wajibu wa serikali ikisaidiana na asasi za kiraia kutoa elimu kwa wananchi bila kusahau viongozi na vyombo vinavyofanya maamuzi juu ya rasilimali za nchi kuhakikisha wanatetea masilahi ya wazalishaji wadogo wadogo.

## Serikali inatakiwa iangalie maeneo ya kupeleka uwekezaji



*Samuel.B.Ngassa (Mkazi wa Kigamboni, DAR ES SALAAM )*


Mfumo wa sasa wa uwekezaji umelenga hasa ardhi ya kijiji. Serikali inatakiwa iangalie maeneo ya kupeleka uwekezaji isiwe katika maeneo yenye rutuba ambapo wanakijiji wanategemea kwa chakula kuhakikisha uhakika wa chakula. Pia, ushirikishwaji wa wananchi kwenye maamuzi ya rasilimali za nchi ni muhimu sana na lazima mfumo wa fidia uwe wa haki na kwa wakati. Ili nchi iweze kuendelea ni lazima zana za kilimo zitolewe kwa wanavijiji ikiambatana na elimu ya mabadiliko ya tabia nchi.



## MKUHUMI ni mfumo mzuri unaoambatana na vipingamizi kwenye utekelezaji

*Kombo Rashid (Mwananchi DAR ES SALAAM)*

Swala la kupunguza hewa ya ukaa kwa kupitia mradi wa MKUHUMI ni mfumo mzuri unaoambatana na vipingamizi kwenye utekelezaji. Tatizo ni kwamba, miradi kama hii mara nyingi hutokana na maamuzi ya vyombo vya juu au shinikizo la wafadhili wa nje. Swala kama hili linaporudi kwa mwananchi linakutana na vikwazo kwa sababu walengwa wakuu (wanakijiji) wanahusishwa kwenye utekelezaji tu na sio kuanzia mwanzo kwenye maamuzi. Ni lazima wanakijiji wenyewe wahusishwe kwenye kupanga au kujadili miradi mbali mbali inayowahusu. Serikali na asasi za kiraia zinapaswa kutoa elimu kwa jamii hasa kwenye maeneo ya miradi kuhusu maana na athari tarajiwa za miradi hii na kuweka bayana manufaa ya wananchi kutokana na miradi husika.



*Uwiano kati ya mahitaji ya wenyeji na hifadhi ya mazingira kama hii uzingatiwe katika biashara ya hewa ya ukaa*

# Kukosekana kwa uwiano wa maslahi kichocheo cha migogoro kwenye uwekezaji



Na Saad Ayoub

Uwekezaji kwa upana wake ni kitu kizuri katika kukuza uchumi wa nchi yoyote ile lakini unaweza kuleta madhara endapo hautafuata taratibu na sheria zilizowekwa katika nchi. Kutokueleweka kwa sheria zinazosimamia uwekezaji kwa upande wa wananchi hasa wa vijijini na ukiukwaji wa sheria hizo na wawekezaji kwa upande mwingine kumekuwa kichocheo cha migogoro baina ya makundi hayo. Kwa mfano tumeona migogoro mingi katika uwekezaji kwenye rasilimali ya madini katika maeneo ya Kahama, Geita, Tarime, Bulyahulu na Mererani.

Vile vile kumekuwepo na migogoro mikubwa baina ya wawekezaji wakubwa na wadogo na wanavijiji katika maeneo ambayo uwekezaji katika ardhi umeshika kasi. Manthalani maeneo ya wilaya za Kisarawe, Kilwa, Bagamoyo, Babati, Kilombero na Rufiji. Hii yote ni migogoro inayosababishwa na ukiukwaji wa misingi muhimu ya uwekezaji ambapo wananchi wamekuwa wakilalamikia wawekezaji kuwa wanapewa ahueni ya kodi, wanasaidiwa kupata ardhi na hati na wanapewa motisha nyinginezo.

Pamoja na migogoro hii kuwepo kwa muda mrefu bado aina tofauti za uwekezaji zinazidi kuingia nchini na katika rasilimali zile zile. Katika miaka ya karibuni kumeingia uwekezaji katika sekta ya upandaji miti kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Uwekezaji huu ambao chanzo chake ni uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile viwanda, ukataji wa miti kwa matumizi ya uchomaji mkaa na uvunaji wa magogo ulitarajiwa uwe na sura tofauti kwa vile umekuja karibuni kulinganisha na uwekezaji katika sekta kama madini ambao umeanza muda mrefu. Fikra za unafuu wa uwekezaji huu zinatokana na hisia kwamba mafunzo juu ya makosa yaliyofanywa wakati wa kuingia mikataba ya madini, uvunaji magogo, uwindaji wa wanyamapori na mashamba makubwa yangerekebishwa. Hata hivyo, kwa maeneo ambayo miradi mikubwa ya upandaji wa miti imeshaanza kutekelezwa, inaelekea serikali imeshindwa kujinasua kwenye mtego wa kuwianisha mahitaji na maslahi ya wananchi wenye ardhi na wawekezaji. Kwa mfano kumekuwa na uchukuwaji mkubwa wa ardhi ya vijiji kwa ajili ya upandaji wa miti, ardhi ambayo ilikuwa ikitumika kwa kilimo cha chakula na ufugaji. Hili peke yake limeshazua migogoro kwa baadhi ya maeneo kama Chogo, Uchindile, Idete wilayani Mufindi na sehemu kubwa ya vijiji vya wilaya ya Kilolo ambako uwekezaji kama huu unafanyika hasa katika vijiji vya Kidabaga, Kimala, Magome, Kising'a na Ukwega.


Eneo la pili na nyeti zaidi ni pale ambapo masharti ya kufaidika na gawio la tathmini ya miti inayonyonya hewa ya ukaa yamekuwa magumu yasiyoruhusu wazalishaji wadogowadogo kuingia katika biashara ya hewa ukaa moja kwa moja. Na hili linaweza kueleweka tu kwa mtu kujiuliza kwanini makampuni yanatafuta kumiliki ardhi yenyewe badala ya kuwawezesha wanavijiji kupanda miti ili yabaki kuwa wanunuzi wa hewa ya ukaa.



Na Happy George

Ndiyo maana hata hiyo asilimia 10, inayolipwa na makampuni kama gawio kwa wanakijiji imekuwa ikilalamikiwa kuwa haina tija wala haiendani na thamani wala kiwango cha ardhi kubwa wanayoiacha kwa ajili ya mwekezaji.

Wakati tukitafakari juu ya athari za migogoro kati ya wawekezaji na wananchi ambayo kama tulivyosema imekuwa ikiripotiwa takribani kila siku hasa kutokana na kukosekana kwa uwiano wa maslahi kati ya pande hizi mbili, ni vema nchi ikawekeza katika mfumo endelevu wa kujenga uelewa wa kijamii juu ya masuala ya uwekezaji, mbinu za ushawishi, utetezi na uingiaji mikataba ili kuepusha athari za migogoro inayofukuta hivi sasa kabla haijalipuka kwa kiwango kisichoweza kudhibitiwa. Hii inatokana na ukweli kuwa, kwavile uwekezaji unafanyika kila mahali hata migogoro inapotokea uwezekano mkubwa ni kwamba itatokea kila mahali. Tunayo nafasi ya kurekebisha sasa kwa kufanya vizuri katika mikataba inayoandaliwa hasa katika sekta hii ya misitu ya kibiashara maana bado ni jipya.



*Uchimbaji mkubwa na mdogo wa madini kama huu unachangia kuharibu mazingira*

# HAKIARDHI ARDHI NI UHAI




**Anuani/Ofisi**
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**, Kitalu Na. 236 Sinza Mori
S.L.P. 75885, DSM, Tanzania. Simu +255 22 2771360 /Faxi +255 22 2771362, +255 784 646 752.
Baruapepe: info@hakiardhi.org Tovuti: www.hakiardhi.org

## MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 2. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 3. | Haki za Wamaasai waishio Hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga |
| 4. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 5. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika |
| 6. | The Silences in the NGO Discourse - Occasional Paper No. 1 - May, *2006* | Issa G. Shivji |
| 7. | The Mute Plunder 'Bioresources & dispossession in Tanzania 2008 | Ng'wanza Kamata |
| 8. | Public Perceptions on Bio Resources Conservation in Tanzania Occasional Paper No. 2 - Julai, *2008* | HAKIARDHI |
| 9. | Accumulation by Land Dispossession and Labour Devaluation in Tanzania 2011 | HAKIARDHI |
| 10. | Maswali na Majibu yanayohusu mfumo wa milki na usimamizi wa ardhi nchini "Kitini cha Kujielimisha" 2011 | HAKIARDHI |
| 11. | Mwongozo wa mafunzo juu ya sheria za ardhi na utawala katika muundo wa Serikali za mitaa 2011 | HAKIARDHI |
| 12. | Maswali na Majibu yanayohusu Migogoro ya Ardhi nchini - 2011 | HAKIARDHI |
| 13. | Land Grabbing in a Post Investment Period and Popular Reactions in the Rufiji River Basin, Occasional Paper No 3- 2011 | Abunuwasi Mwami & Ng'wanza Kamata |
| 14. | Kilimo kwanza na nafasi ya mzalishaji mdogo nchini Tanzania-2012 | HAKIARDHI |